# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 11 Juni, 2019

*(Bunge Lilianza Saa 03:00 Asubuhi)*

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Roman Selasini.

Na. 355

**Umuhimu wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. HAMIDU H. BOBALI)** aliuliza:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba Serikali ni pamoja na Serikali za Mitaa na mtu yeyote anayetekeleza madaraka au mamlaka kwa niaba ya Serikali au Halmashauri.

Je, kwa nini katika kipindi chote cha uwepo wa Katiba hiyo Serikali haijatunga Sera ya Ugatuaji Madaraka ambayo ingewezesha kuweka mfumo wa kisheria unaoelekeza mipaka, majukumu na utaratibu wa utekelezaji wa matakwa hayo ya Kikatiba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Jimbo la Mchinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali za Mitaa zipo kwa mujibu wa Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mwaka 1998 Serikali iliandaa andiko la kisera la maboresho ya Serikali za Mitaa ambalo ndio mwongozo wa utekelezaji wa Sera ya Ugatuzi wa Madaraka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hata hivyo, kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Sera ya Taifa ya Ugatuzi wa Madaraka ambayo inatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2019/2020. Sera hiyo itaweka mfumo wa kisheria unaoelekeza majukumu na mipaka ya wadau mbalimbali kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika utoaji wa huduma kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Roman Selasini swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu ambao ni kinyume cha Sheria Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Makatibu Tarafa na hata Watendaji wa

Kata kuwafukuza Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji papo kwa papo kwenye mikutano ya hadhara.

Je, Serikali ina tamko gani kuhusu jambo hili ambalo ni kinyume cha sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kwamba Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana wakiwasaidia Madiwani na Wabunge na kwa kweli ndiko Serikali za wananchi ziliko, lakini wamekuwa hawapati posho, posho zao zinasuasua, hawapati mishahara, wamekuwa wakifanya kazi kwa taabu sana.

Je, Serikali inasema nini hasa katika hiki kipindi cha Bajeti kuhakikisha kwamba watu hawa wamepata posho kidogo kwa ajili ya kuwasaidia kufanya kazi zao kwa ufanisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba ni-*declare interest* kwamba na mimi pia kuanzia mwaka 2014 hadi 2017 nilikuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kivule, Ukonga - Dar es Salaam, swali lake la kwanza anaulizia juu ya namna ambavyo Wenyeviti wa Vijiji Vitongoji na Mitaa wanavyoondolewa madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria, kwanza kama unataka kumuondoa Mwenyekiti wa Kijiji, hayo maeneo niliyoyataja, la kwanza ni lazima wapatikane watu ambao wana watuhumu hao viongozi katika eneo lao la kiongozi ambalo wamechaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili lazima hao watu waandike malalamiko kwa maandishi wampelekee Mkuu wa Wilaya wakitaja tuhuma moja baada ya nyingine ambayo muhusika na mlalamikiwa ametenda na jambo la tatu ni lazima Mkuu wa Wilaya au anayehusika ataandika

maana yake sheria inamtambua Mkuu wa Wilaya kwenye ngazi ya Wenyeviti wa Vijiji kuja chini, atamwandikia Mwenyekiti wa Kijiji, Kitongoji au Mtaa tuhuma zake kwa maandishi, ndani ya muda usiozidi siku saba mtuhumiwa atalazimika kujibu tuhuma alizopewa na baada ya hapo, baada ya kupokea majibu ya tuhuma zile Mkuu wa Wilaya ataitisha mkutano wa wananchi wa eneo husika na sheria inasema watakao hudhuria siyo chini ya nusu ya wakazi wa eneo husika na wawe wamekuwa *registered* kwenye *registration* ya mtaa husika wanaotambulika, watu wazima wenye akili timamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo watapewa nafasi ya kujitetea mbele ya mkutano huo, atasomewa tuhuma zake, atapewa nafasi ya kujitetea na baada ya hapo wananchi baada ya kumsikiliza watapiga kura sasa kuonesha kwamba hawamtaki, mbili ya tatu (2/3) ya mkutano uliohudhuriwa wakikubali kwamba hafai ataondolewa madarakani na huo ndiyo utaratibu na naomba viongozi wazingatie muongozo huo wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni habari ya posho au mishahara kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji. Swali hili nimejibu mara nyingi, naomba nirudie; kwa mujibu wa sheria hizi kazi, zetu hizi, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji hawapewi mishahara, lakini hata hivyo kwa sababu ya kuangalia umuhimu wa shughuli ambazo wanafanya na unyeti na ni kweli wanafanya kazi zaidi ya masaa 24 sheria imeelekeza na TAMISEMI tumeelekeza, naomba nielekeze pia kulingana na mapato ya Halmashauri kwenye eneo husika Wakurugenzi wetu wamekuwa wakipanga namna ya kuwapa posho za kujikimu, kuweza kulipia ofisi zao, kuwapa vitendea kazi ikiwepo na *photocopy.* Maeneo mengine kulingana na mapato yao wamepanga wanalipwa shilingi 50,000 kwa mwezi, kule Dar es Salaam najua wanalipwa shilingi 100,000 kwa mwezi, kwa hiyo, inategemea na mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sheria haijabadilishwa na Waheshimiwa Wabunge Bajeti ya

TAMISEMI imeshapitishwa na kwa kweli hatukupokea maoni yoyote ya Halmashauri wakitaka kupandisha posho za Wenyeviti wa Mitaa au wa Vijiji, hili jambo tulipokee, tutafakari kwa pamoja tukipata uwezo tuboreshe utaratibu huu ili Wenyeviti wa Mitaa waweze kulipwa kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, wanatusaidia sana katika kazi hii na wanafanya kazi ya kipolisi, mahakama, kifamilia na mambo mengi kadha wa kadha ambayo yanafanyika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amejibu mimi kwanza nimpongeze kwa majibu yake mazuri, lakini bado kuna tatizo la hawa watendaji wetu yaani kwa maana kwamba Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani ni kwamba hawajapata semina, pamoja na kwamba sheria/sera bado haijaletwa ya ugatuzi wa madaraka lakini bado uko umuhimu wa kuwapa semina mara kwa mara ili waweze kujua mipaka yao ili waweze kuboresha utendaji wao wa kazi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa semina hawa watu, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji ili waweze kufanya kazi vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuna maeneo hawa viongozi hawajapata semina lakini ninachojua na maelekezo ya TAMISEMI ambayo na mimi nimesema nilikuwa Mwenyekiti wa Mtaa tulifanyiwa baada ya uchaguzi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa wale viongozi wakishapatikana kabla ya kuanza kazi wanapewa semina ikiwa ni pamoja na kuapishwa, hawa

wajumbe wanakula viapo vya uaminifu kwenye ngazi ya Halmashauri na wanapaswa kuapishwa na Mwanasheria Mkuu wa Halmashauri husika, hilo linapaswa kufanyika, kama kuna mahali halikufanyika nitaomba kwa sababu tunaenda kwenye uchaguzi wa mwaka huu tutalisimamia ili viongozi wakishapatikana wapate semina, waapishwe lakini kubwa zaidi ni lazima wajue mipaka yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako majukumu na kuna tofauti kubwa kwa mfano ya Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa ni waratibu wa shughuli za Serikali za Mitaa, wakati Wenyeviti wa Vijiji ni Serikali kamili wana maamuzi wanaweza hata wakachukua rasilimali za eneo fulani wakauza wakafanya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hayo mambo tutayasimamia ili yaweze kufanyiwa kazi na naomba viongozi wetu wa Halmashauri na Mikoa wajipange, baada tu ya uchaguzi haitakiwi Mjumbe wa Serikali ya Mtaa au wa Kijiji au Mwenyekiti aanze majukumu yake bila semina, kiapo na mafunzo tutayazingatia na chuo chetu kikuu cha mafunzo ya Serikali za Mitaa za Hombolo kina nafasi hiyo na hata nyie Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa hata sasa mkitaka na wajumbe wenu mnawapeleka pale, tuna nafasi ya kutosha walimu waliobobea, karibu Hombolo Chuo cha Serikali za Mitaa wapate mafunzo ili wafanye kazi kwa kuboresha huduma za kijamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kuna baadhi ya Wenyeviti katika vijiji vyetu baada kuteuliwa tu baada ya miezi mitatu/minne wanajiuzulu wengine wanafariki, lakini hakuna chaguzi zinafanyika na mfano hasa kwenye Wilaya yangu kunakaa wazi, wanateuliwa tu mtu anakaimu anakuwa pale, sasa demokrasia inasemaje kuhusu watu wanaojiuzulu na wanaofariki kwa nini uchaguzi haufanyiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kweli, nimesikia sikia naomba nitoe maelekezo, kwanza, hakuna mtu anaitwa Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji, Kitongoji au Mtaa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, haipo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika ni kwamba Wajumbe na kuna watu wengine mtu akijiuzulu anakaimu kwa muda mrefu na anatembea na muhuri kwamba ni Mwenyekiti, hilo zoezi kama lipo kuanzia sasa na leo muda huu, likome halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika mtu akijiuzulu Wajumbe wa Serikali ya Mtaa wanapokutana kwenye kikao, miongoni mwao anakuwa Mwenyekiti wa kikao hicho na uenyekiti wake unakoma mara tu baada ya kikao kuisha wakati ule, anayepaswa kufanya kazi ya kiutendaji ni Mtendaji wa Kijiji au Mtendaji wa Mtaa mpaka uchaguzi ufanyike, lakini uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wakati wowote ikitokea *gap* tunategemea kupata taarifa kutoka ngazi ya Kijiji au Mtaa inakuja TAMISEMI, tunaruhusu wafanye uchaguzi kwa sababu kwanza unasimamiwa na eneo husika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu akijiuzulu, kwa mfano mwaka mmoja kabla ya Uchaguzi Mkuu kama sasa, hatukuruhusu kwa sababu sheria inazuia huu muda hauruhusiwi, lakini muda wowote wa nyuma Mheshimiwa Ally Keissy kama ilitokea ni bahati mbaya sana na tunaisimamia tupate taarifa baada ya uchaguzi huu, kama inatokea mtu amejiuzulu baada ya muda siyo mrefu sana inabidi achaguliwe ili wananchi wahudumiwe na mtu ambaye wamempigia kura, waweze kumwajibisha kwa ile imani waliyompa. Ukikaimisha mtu ambaye hawakumchagua wao watashindwa kumwajibisha na ukienda kumuhoji anasema

mimi siyo Mwenyekiti nilikuwa nakaimu na anakimbia majukumu yake. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la pili Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli Mbunge wa Lupembe sasa aulize swali lake.

Na. 356

**Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata yamekuwa ni chanzo cha migogoro badala ya kutatua migogoro.

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kutoa mafunzo ya muda mfupi ili waweze kumudu majukumu yao kwa ufanisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Kata ni vyombo vya kisheria vya utatuzi wa migogoro katika ngazi ya chini ya jamii vyenye nguvu ya kisheria katika kutatua migogoro ya wananchi. Mabaraza hayo yaliyoanzishwa mwaka 1985 kwa Sheria ya Mabaraza ya Kata, Sura ya Namba 206 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika utekelezaji wa majukumu yake, baadhi ya Mabaraza yamekuwa na changamoto za kiutendaji zinazotokana na

uelewa mdogo wa masuala ya kisheria kwa wajumbe, maadili na kutofahamu mipaka ya majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilitoa mafunzo kwa Wanasheria wa Halmashauri kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Mabaraza ya Kata. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ilitoa mafunzo kwa Wakurugenzi na Wanasheria wa Halmashauri. Mpango wa Serikali ni kuendelea kutoa mafunzo kwa Mabaraza hayo kadri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joram Hongoli swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la kuingiliwa katika maamuzi ya kesi na wanasiasa hasa kwenye maeneo ya vijijini na hivyo kuathiri yale maamuzi.

Je, Serikali inatoa maelekezo gani kwa maeneo hayo ya vijijini ambako kumekuwa na mwingiliano wa viongozi wa kisiasa hasa Madiwani?

Lakini pili kumekuwa na tatizo kubwa la Mabaraza haya kutokuwa na vifaa vya kufanyia kazi, lakini kutokuwa na ofisi, posho za kuweza kujilipa na mwisho wa siku imekuwa wakiona yule anayedaiwa au anayehukumiwa ndiyo mwenye uwezo, wanaangalia nani mwenye uwezo basi wanamu-*award* ili waweze kupata hizo fedha na mwisho wa siku waweze kujilipa au kuweza kununua hivyo vifaa?

Je, ni nani mwenye wajibu wa kutoa hivi vifaa na kutoa hizi posho lakini pia na ofisi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya wanasiasa ambao wanaingilia mambo hayo ya uendeshaji wa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza kwenye jibu langu la msingi, haya mambo ni mambo ya kisheria ya tangu mwaka 1985 na yamefanyiwa marejeo mwaka 2002 wale Wajumbe wa Mabaraza ya Kata ni Wajumbe ambao wanatoka kwenye Kata husika kwa hiyo lazima uwe mkazi wa Kata husika kama siyo mkazi hupaswi kuingia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili la kuangalia wakati unapata Wajumbe wa Uendeshaji wa Mabaraza ya Kata, ni lazima hao watu wasiwe na tuhuma zozote za jinai na makosa mbalimbali kwa lugha nyingine lazima wawe ni waadilifu katika eneo lile, lakini majina haya ambayo yanaombwa yanapaswa kubandikwa kwenye *notice* za matangazo ili kama kuna mwananchi ana pingamizi dhidi ya mtu yeyote mjumbe aliyeomba aondolewe, lakini hakuna nafasi kabisa ya kiongozi wa kisiasa kuingilia kwa sababu kuna Kamati ya *Ward DC* inapendekeza majina kwa maana ya maoni, lakini uteuzi wa mwisho wa wajumbe hawa unafanywa na Halmashauri akiwepo Mwanasheria wa Halmashauri na Mkurugenzi na viongozi wengine, na ikiwezekana Mkuu wa Wilaya anaingia katika eneo hilo kwa maana ya kufanya *consultation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mujibu wa sheria hakuna namna ya kuingilia, lakini kama kuna eneo ambalo viongozi wa kisiasa wanaingilia hayo ndiyo maeneo tunayohitaji kupata taarifa ili tuweze kuchukua hatua na kutoa maelekezo na kuendesha vizuri katika maeneo hayo bila kuingiza siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni vitendea kazi ambayo inapelekea pia maamuzi ambayo yameyumbishwa kulingana labda na vipato na kuangalia nani amepeleka kesi katika eneo hili. Ni kweli kwamba tumepata pia maneno maeneo mbalimbali wanakosa vitendea kazi, lakini haya Mabaraza yanasimamiwa na Wakurugenzi wa Utendaji wa Halmashauri na Wanasheria wa Halmashauri na ndiyo maana baada ya kuchaguliwa wanapaswa waende watoe semina na mafunzo, lakini Bajeti za Halmashauri lazima ziwe na kipengele ambacho kinasaidia uendeshaji wa Mabaraza haya ya Kata na hata fedha ambazo wanapanga kwa mfano kesi imeamuliwa kutoka eneo moja ofisini kwenda kuangalia mahali ambapo kuna malalamiko inabidi gharama ile iwe ni gharama iwe ni gharama ya kawaida kabisa ndogo ambayo mtu wa kawaida ataifanya, na lengo la Mabaraza haya ni kupunguza umbali wa kuwafanya wananchi kutoka kwenye Kata yake kwenda kwenye Mahakama za mwanzo na Wilaya, lakini vilevile kuwasaidia watu wa kawaida kabisa ngazi ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nielekeze Wakurugenzi Watendaji na Wanasheria katika Halmashauri zetu kama kuna maeneo kuna malalamiko makubwa na watu wanakuwa *charged* gharama kubwa, naomba wachukue hatua ili tuweze kusimamia, tuweke viwango vya kawaida kabisa ambavyo mtu wa kawaida anaweza kufanya, lakini mwisho isije ikatokea hata siku moja kwa sababu kuna mtu ana malalamiko yake na kwa sababu hana uwezo wa kifedha asisikilizwe hili litakuwa ni kosa kwa viongozi wetu ambao wanasimamia katika eneo lile na itakuwa inaenda kinyume kabisa na maelekezo ya Baraza na Uanzishwaji wa Baraza la Usuluhishi wa Kata, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba unisikilize vizuri.

Kwa kuwa ni-*declare interest* kwamba niliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya kwa hiyo najua matatizo ya Mabaraza ya Kata. Mara nyingi wanaolalamika ni wale ambao hawana uwezo, ndiyo wanadhulumiwa ardhi na mashamba yao, wanaowadhulumu ni watu wenye uwezo na kwa sababu Halmashauri hazina uwezo wa kifedha wanaotoa gharama ya kuendeshea kesi hizo mahakama hiyo ni wale waliolalamikiwa wenye fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri haki itapatikana? Mimi nafikiri naomba unijibu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais,TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, haki inapaswa kupatikana hata kama hauna pesa, maelekezo ni kwamba zile bei ni kweli wanakubaliana, kwanza bahati nzuri viwango vya kutoza ni viwango ambavyo kwenye ngazi ya Kata ya Diwani na *Ward DC* yake wanaweza ku-*moderate,* Halmashauri zinaweza kusimamia, Mkuu wa Wilaya anaweza kuingilia, Mkuu wa Mkoa anaweza kuingilia, kwa hiyo, kuna *flexibility* kubwa sana ambayo unaweza ukaangalia hapo, lakini mahali pengine ilipotokea tumetoa maelekezo isitokee mtu ambaye hana uwezo asitendewe haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapanga viwango vya kawaida na maeneo mengine tumetoa maelekezo unakuta kwamba kwa mfano hata hukumu imetoka, lakini ile gharama ya kwenda kuchapisha ni kubwa anatozwa mwenye kesi, ikikosa anapeleka mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nitoe maelekezo ni kwamba hili jambo ni jambo muhimu, jambo la

kisheria na lililenga kimsingi kusaidia watu wa ngazi ya chini au maskini ndiyo Mabaraza ya Kata lililenga naomba viongozi wetu wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge tuwasiliane, kama kuna mahali Mheshimiwa Mwamoto kuna mwananchi amedhulumiwa au hakusikilizwa kwa sababu hana fedha nipo tayari twende sasa hivi tukamsikilize na apate haki yake, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 357

**Kupandisha hadhi Barabara ya Mtiri - Mlimba**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Barabara ya Mtiri - Ifwagi - Mdaburo - Ihamu - Mpangatazara hadi Mlimba inaunganisha Wilaya ya Mufindi na Kilombero, na ni muhimu sana kiuchumi na kijamii kwa mikoa hiyo miwili. Aidha, Mheshimiwa Rais aliahidi kuipandisha hadhi barabara hii kuwa chini ya *TANROADS.*

(a) Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi barabara hiyo ili kuwa chini ya *TANROADS?*

(b) Je, kuna mkakati gani wa dharura kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa wakati wote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Ndivyo ilivyo, sauti ya zege mama. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mtiri – Ifwagi - Mdaburo – Ihamu – Mpangatazara hadi Mlimba ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* Wilaya ya Mufindi. Kufuatia kuundwa kwa *TARURA* mwaka 2017 maombi ya kupandishwa hadhi barabara za Wilaya kuwa za Mkoa au kusimamiwa na *TANROADS* kwa kigezo cha kukosa fedha limesimamishwa kwa muda ili kuipatia *TARURA* fursa ya kutekeleza majukumu mahsusi ya kuundwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inayopita kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya biashara na chakula pamoja na kuendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali, barabara hii imewekwa kwenye mpango wa kukarabatiwa kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi ujulikanao kama *Road Inclusion and Social Economic Opportunities (RISE).* Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa swali la nyongeza.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mindombinu ya Bunge ilitoa maelekezo kwa Serikali kwamba iangalie sasa barabara zinazounganisha Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa zipewe kipaumbele za kupandishwa hadhi kuwa barabara za *TANROADS.* Barabara hii mchakato wa kupandishwa hadhi ulianza mwaka 2013, lakini mpaka leo hii kumekuwa kuna maneno haya kwamba tumesimamisha. Nataka nipate tu kauli ya Serikali, sababu zipi zilizopelekea kusimamisha

barabara ambayo tayari mchakato wake ulishaanza mwaka 2013?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mpaka sasa hivi barabara haipitiki kabisa na nimeuliza katika swali langu la msingi, ni hatua gani za dhararu Serikali inaweza kuzichukua ili kuhakikisha barabara hii inapitika.

Sasa maelezo yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Naibu Waziri ni mipango ya muda mrefu. Sasa hivi watu hawapati nafasi ya kupita, watu wanakufa katika maeneo yao, mazao yanaharibika, ni hatua zipi za dharura zitakazosaidia barabara ipitike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Mgimwa kwa sababu barabara hii ameizungumza sana hata wakati akichangia kwenye bajeti ya Wizara, ameizungumza barabara hii. Pia niseme tu kwamba tumekuwa na chombo hiki cha *TARURA* na niseme kwamba *TARURA* imeanza vizuri kwa sababu imefanya kazi kubwa sana kwa muda mfupi. Hivi ninavyozungumza *TARURA* wamemaliza zoezi la kuzitambua barabara zetu ili sasa kuona urefu wa barabara zote kwenye Halmashauri za Wilaya zetu, kuangalia hali za barabara na idadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi linafanyika kuangalia idadi ya magari yanayopita katika maeneo, lengo kubwa ni kuweza kufanya uchambuzi na hivi ninavyozungumza iko kamati maalum ambayo inakaa kule Morogoro itamaliza kazi yake mwezi huu wa Juni, ikiwa na wajumbe kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wizara ya Ujenzi, TAMISEMI, Maliasili na Utalii, *TANROADS, TARURA* wenyewe, Wizara ya Ardhi na Ofisi ya *AG* ili sasa kuweza kuzipanga upya barabara zetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mgimwa naomba uvute subira tu kwamba pamoja na *status* ya barabara pia itatazamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza juu ya maboresho ya haraka kwenye maeneo haya kama hapapitiki. Nafahamu kwamba kipindi kilichopita tumekuwa na mvua nyingi sana na maeneo mengi yamekuwa hayapitiki kwa sababu pia kumekuwa na changamoto hii ya wakati wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuelekeze tu Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Iringa ashirikiane na wenzetu upande wa *TARURA* tuone maeneo ambayo wananchi hawapiti tuweze kukwamua waweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hili nitalifutilia ili wananchi wapite wakati hizi hatua nzuri ambazo nimezitaja za kuiboresha hii barabara ili kuiunganisha kutoka eneo hili la Mufindi kwenda Morogoro kupitia Mlimba liweze kwenda vizuri.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mgimwa naomba uvute subira, natambua pamoja na Kamati kutoa maelekezo lakini hatua za haraka tumezichukua, tutazipanga barabara zetu na hii barabara yako Mheshimiwa Mgimwa tutaitendea haki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dua Nkuruwa swali la nyongeza.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba *TARURA* naikubali na nafahamu uwezo wake lakini ni kwamba kuna maeneo *TARURA* inakuwa na uwezo mdogo ndiyo maana tunakuja na haya maswali.

Sasa nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini barabara kutoka Mangaka hadi Matekwe Wilaya ya Nachingwea mpaka Liwale Wilaya ya Liwale itaweza kupandishwa hadhi kwa sababu tayari Wilaya zote tatu zimeshaombea kupanda hadhi? Naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kama nilivyozungumza muda mfupi kwamba kulikuwa na changamoto ya mgao wa fedha kwa kuzingatia mahitaji ya maeneo husika na hali ya jiografia ndiyo maana baada ya *TARURA* kuwepo tumelazimika kufanya uratibu na kuzitambua barabara zote ili sasa ziweze kupata huduma kadri inavyostahili kutokana na uwiano wa namna pia tunavyopata fedha. Kwa hiyo, hilo zoezi limeenda vizuri na ninaamini kabisa kati ya maeneo ambayo labda wakati mwingine hayakupata *allocation* nzuri, baada ya zoezi hili yatapata mgao kulingana na uwezo wa kifedha, lakini pia kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ya Mangaka - Nachingwea kwenda Liwale zipo hatua kadhaa zinaendelea, kutoka Nachingwea kwenda Liwale kilometa 129 tumeanza usanifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami, lakini nafahamu kutoka Nachingwea kuja Mangaka kwamba liko zoezi wakati wote tumetenga fedha tutaanza ujenzi wa lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dua na kwa vile pia ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu tukutane tu hata baadae pia uweze kuona mpango mzima wa maeneo tulivyojipanga kwa ajili ya kuboresha barabara zetu katika mkoa huu wa Mtwara pamoja na barabara zetu upande wa Lindi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kweli ukizungumza suala la barabara, ukiangalia Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Hongoli wote hawa wanatobozana kwenye Jimbo langu. Hiyo inakuza uchumi ndani ya Mkoa wa Morogoro Wilaya ya Kilombero hususan Jimbo la Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema siku ile nipewe maji hivi sasa hali ya barabara ya Ifakara – Mlimba inapitika kwa magari tu ya mizigo midogo midogo, magari ya abiria hayapiti kwa hiyo kupata taabu sana kina mama ambapo wanakwenda kufuata huduma ndani ya Wilaya ya Kilombero - Ifakara.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kurekebisha ile barabara ya kutoka Mlimba hadi Ifakara ili kina mama na watoto na abiria wengine na mizigo sasa hivi tunavuna ili ipate kupita kwenda sokoni na kupata huduma za jamii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mlimba pamekuwa *special* kidogo kwa sababu yako mahitaji ya kuunganika na Njombe kwa maana ya kutoka kule Lupembe, Madeke kuja Mlimba, lakini iko kiu ya kuunganishwa na Mufindi kama Mheshimiwa Mgimwa alivyozungumza, lakini pia kutoka Kilolo kuja Mlimba. Kwa hiyo, utaona wananchi wa maeneo haya na kihistoria walikuwa sehemu moja na bado shughuli zao za kiuchumi zinafuatana. Niseme tu kuhusu mpango wa dharura wa kutengeneza maeneo haya na Mheshimiwa Susan amerusha picha nyingi sana kuonesha wananchi walivyopata adha nyingi sana wakati wa mvua zikiwa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakubaliana na mimi kwamba wakati wa mvua zikiwa nyingi na maji yakiwa mengi kufanya matengenezo kwenye barabara zetu inakuwa ni ngumu, lakini kwa vile mvua zimepungua na tunazo fedha za *emergency* kwa ajili ya matengenezo. Tumetoa maelekezo kwamba mvua zikipungua mara moja cha kwanza ni kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yameharibiwa na mvua yanarekebishwa ili wananchi waendelee kupata huduma hii ya barabara, huduma muhimu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Susan vuta subira tumea maelekezo na ninarudia kuelekeza wenzetu *TANROADS* Mkoa wa Morogoro baada ya mvua kupungua sasa nguvu kubwa ielekezwe kwenye maeneo ambayo wananchi wamepata shida wakati wa mvua kubwa zilizonyesha hivi karibuni. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shaabani Shekilindi swali la nyongeza.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya kuanzia Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya – Milingano hadi Mashewa iliombewa kupandishwa hadhi toka mwaka 2009 sambamba na barabara ya Dochi hadi Mombo.

Je, ni lini barabara hizi zote mbili zitapandishwa hadhi ili wananchi wangu waweze kuondokana na adha wanayoendelea kuipata sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi al-maarufu kama *Bosnia* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara alizotaja Mheshimwa Mbunge yaani kwa maana ya ile barabara ya kutoka Mlalo kwenda Makanya na hii barabara ya Dochi, kama nilivyozungumza kwamba kamati maalum inaendelea na kikao kufanya mapitio ya kuweza kurekebisha na kuweka hadhi za barabara zetu zote nchini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Shekilindi naomba avute subira, baada ya zoezi hili tutamfahamisha kwamba barabara zake hizi zime-*meet* vigezo ili tuone kama zinaweza kupandishwa hadhi, lakini lazima shughuli za kitaalum zifanyike kabla ya hatua ya

kupandisha hadhi barabara hii, kwa hiyo, vuta subira muda siyo mrefu utapata majibu yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba tu kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri. Tatizo la barabara la Dutwa – Imalamate – Ngasamo kwenda mpaka Nyashimo lilikuwa kwenye ahadi ya Mheshimiwa Rais na huu ni mwaka wa nne kwamba iwe kwa kiwango cha lami.

Nilitaka tu kujua, ni lini sasa barabara hii itawekewa lami kulingana na ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amefuatilia sana hii barabara, kwa hiyo hata nikikutana naye nje huwa namwita Mzee wa Nyashimo kwa maana ya umuhimu wa barabara hii. Nafahamu pia Mheshimiwa Chenge anaizungumza sana barabara hii, lakini nafahamu pia kwamba iko ahadi ya Mheshimiwa Rais. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Chegeni kwamba ahadi zote za viongozi tunaendelea kuzitekeleza, kadri tunavyopata fedha tutatekeleza ahadi za viongozi.

Kwa hiyo, ahadi ni deni na usiwe na wasiwasi na mimi naifuatilia sana barabara hii kwa umuhimu wake ili tuweze sasa kwenda kwenye kujenga katika kiwango cha lami, tukipata fedha tutakwenda kujenga barabara hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 358

**Ujenzi wa Madaraja Gairo – Chakwale – Idilo – Kilindi**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, ni lini madaraja ya barabara ya Gairo – Chakwale – Idilo – Kilindi yatajengwa au kukarabatiwa ili barabara hiyo iweze kupitika wakati wote wa masika na kiangazi bila matatizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Gairo – Chakwale – Idilo – Kilindi ni barabara ya mkoa inayounganisha Wilaya ya Gairo iliyopo Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Kilindi iliyopo Mkoani Tanga. Sehemu ya barabara hii kwa upande wa Mkoa wa Morogoro inaitwa Iyogwe – Chakwale – Ngilori (kilometa 42) na sehemu iliyobaki ya kutoka Iyogwe – Kilindi iko Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii hususan katika wakati wa kusafirisha mazao ya kilimo na chakula kwa Wilaya ya Gairo na Kilindi, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imetenga kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *vented drift* moja na *box culverts* mbili kwenye mito mikubwa ya Chakwale, Nguyani na Matale iliyoko katika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pia naipongeza Serikali kwa kutenga shilingi milioni 100 kwa kuanza matengenezo haya ya barabara ya Iyogwe – Chakwale – Ngilori. Barabara hii ni muhimu sana na hasa kwa upande wangu naona ni muhimu sana kwa upande wa jamii pamoja na uchumi. Nikisema jamii ni kwa sababu wakati wa kipindi cha mvua inakuwa matatizo kupitika hii barabara. Mto huu wa Chakwale, Nguyani na Matale mpaka sasa hivi zina *drift culverts,* lakini inakuwa muhimu sana na inakuwa matatizo kwa sababu maporomoko ya maji yanakuwa mengi sana wakati wa mvua kiasi wanafunzi wanashindwa kupita na magari.

Je, nauliza Serikali kwa sababu mpaka sasa hivi kuna *drift culverts* ambazo bado matatizo, kwa nini haikufikiria kuwa iweke *box culverts* kwa mito hii mikubwa yote mitatu ya Chakwele, Nguyani pamoja na Matale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara ya Gairo – Enongwe pamoja na barabara ya Mzumbe – Mgeta ni barabara muhimu sana kwa mazao ya mboga mboga. Barabara hizi zina ahadi za Mheshimiwa Rais kwa kutengeneza kwa kiwango cha lami; Je, ni lini barabara hizi zitaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami? ahsate. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli

kwenye barabara hii ni barabara ambayo ina changamoto. Mimi nimeitembelea barabara hii, nimeona maeneo haya anayataja Mheshimiwa Mbunge, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hivi karibuni alitembelea eneo hili akajionea changamoto ambazo zipo. Kuna maeneo korofi kwa mfano eneo la Nguyani ambalo tunasema tutaweka *drift* daraja ili iweze kutusaidia wakati ule mpango mkubwa wa kufanya *box culvert* kubwa inatengenezwa pale.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tatizo la eneo hili tunalitambua, wapo watu ambao wamepoteza maisha katika eneo hili, ukienda eneo hili la Nguyani wanapaita ni mto kaburi kwa sababu ya historia kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tunalitambua hili na niseme katika bajeti yetu ya mwaka huo unaokuja ziko fedha ambazo tumezitenga kwa ajili ya kushughulikia maeneo korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sambamba na kuweka hii *culvert,* lakini pia tunaitazama kwa mapana kwa sababu Mheshimiwa Mbunge wa eneo la Gairo tumekubaliana tutafuatana naye pamoja na Katibu Mkuu kwa sababu ya kuona namna ya kwenda kwa haraka kuwarekebishia wananchi hawa.

Kwa hiyo, nikutoe hofu kwamba eneo hili tunalifahamu na tunachukua hatua, na kupitia fedha ambazo Bunge hili limetupitishia yapo maeneo pia ambayo tuna *allocation* ya fedha kwa maana ya kushughulikia maeneo korofi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na kiasi cha fedha tulizotenga, lakini jicho la pili linatazama eneo hili tuweze kuliboresha ili wananchi tuwaokoe kwenye hatari waliokuwa wanaipata, lakini waweze kupita kwenda kwenye shughuli za kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais barabara unayoitaja ya Mzumbe – Mgeta kama nilivyozungumza, ahadi zote za viongozi wakuu ikiwemo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu tutaendelea

kuzitekeleza. Katika Mkoa wa Morogoro yako maeneo ambayo utekelezaji wake wa ahadi hizi uko karibu asilimia 100. Kwa hiyo, uone kwamba tunakwenda hatua kwa hatua, kwamba baada ya kufanya utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais kwenye baadhi ya meneo kwenye Mkoa wa Morogoro, itafika zamu ya eneo hili tutakwenda kufanya matengenezo kulingana na ahadi ya kiongozi mkuu Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Desderius Mipata swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa NaibU Spika, barabara mbili katika Jimbo la Nkasi Kusini zinazounganisha Makao Makuu ya Kata, Kata ya Kizumbi barabara ya Wampembe Junction - Kizumbi na barabara ya kwenda Makao Makuu ya Kata ya Ninde zote zimevunjika, madaraja yamevunjika na sasa hazipitiki kabisa na barabara ya Kizumbi tuliweza kumpeleka Mheshimiwa Waziri Jaffo alipotutembelea lakini bado mpaka sasa tunafuatilia sana hatujapata hizo pesa.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba barabara hizi zinafunguka na wananchi wa Kata hizi wanafikiwa kwa huduma mbalimbali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu utaratibu wa matengenezo wa barabara zetu kupitia fedha ambazo zinatoka kwenye mfuko wa barabara ambao unapeleka fedha *TANROADS* na kupeleka fedha pia upande ule wa *TARURA,* utaratibu ni kwamba asilimia 90 ya fedha zote zinakwenda kwa ajili ya kurejeshea miundombinu hii kwa

maana ya matengenezo na asilimia 10 ndiyo inakwenda kwa ajili ya ujenzi wa barabara mpya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mipata sijafahamu sawasawa labda baadae tuzungumze tuone kama hii barabara iko chini ya *TARURA* kwa sababu mmemtembeza Mheshimiwa Jaffo, lakini sisi kama Wizara ya Ujenzi tunashughulikia sera hii ya barabara, tunao wajibu wa kushirikiana na wenzetu upande wa TAMISEMI, kwa hiyo tuione, lakini kikubwa ni kwamba nimuombe tu Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Rukwa aweze kuwasiliana na wenzake upande wa *TARURA* tuone kwamba eneo hili nani analishughulikia, lakini ni muhimu kwamba eneo hili lishughulikiwe mapema. Naelekeza kwamba lishughulikiwe mapema haya madaraja yatazamwe yarekebishwe ili wananchi wapate huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitatazama kwa makini eneo hili na saa nyingine utanipa *details* za kutosha ili tushughulikie eneo hili wananchi wako wasipate shida na najua wanayo hamu ya kupita katika maeneo haya kwa sababu maeneo haya yana uzalishaji mkubwa sana hasa mazao ya kilimo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha Nachuma, swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matengenezo ya mara kwa mara ambayo hayakidhi haja ya barabara kubwa inayotoka Mtwara Mjini mpaka pale Mnazi Mmoja, Manispaa ya Lindi kwa sababu barabara hii imekuwa inaharibika sana kwa magari yanayosafirisha saruji kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam na Serikali inaahidi kutengeneza kwa kiwango kikubwa lakini mpaka leo barabara hii ina mashimo, wanaweka viraka vidogo vidogo lakini hairekebishwi vile ambavyo inatakiwa kujengwa.

Je, ni lini Serikali inatekeleza ahadi yake ya kutekeleza na kutanua barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara Mjini mpaka Mnazi Mmoja na kule Nanganga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ya kutoka Mtwara kuja Mnazi Mmoja - Mingoyo inatumika sana na magari makubwa ambayo yanabeba mzigo mkubwa hususan saruji, na ni kweli barabara hii nimeipita ina mashimo na tunaendelea kuyaziba hayo mashimo ili huduma iweze kurejea, lakini Mheshimiwa Mbunge utakubaliana na mimi kwamba barabara hii imedumu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zina umri wake na barabara ndiyo maana zinaendelea kuhudumiwa lakini barabara ukiikuta imekaa zaidi ya miaka 30 inastahili sasa hiyo barabara tuibadilishe kabisa kwa sababu ndiyo maana unaona ukiziba hapa sehemu nyingine inafumuka kwa sababu ule muda wa kuishi wa barabara hii umetimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba uko mpango kabambe ambao tutakuwa na mradi wa *World Bank* ambao taratibu zinaendelea vizuri kwamba tutaifanyia matengenezo na kuijenga upya barabara hii kutoka Mtwara kuja Mnazi Mmoja kwa maana hiyo na kutoka pia Mnazi Mmoja kwenda mpaka Masasi kwa hiyo upo mradi unaendelea vizuri. Kwa hiyo wewe uwe *comfortable* hatua zinaenda vizuri. Wakati ukifika utaona tunaenda kufanya maboresho makubwa ya barabara hii muhimu na mahitaji ya matumizi ya barabara hii sasa hivi yameongezeka sana, hali ya Mtwara sio kama zamani, utakubaliana na mimi kwamba tunaitazama kwa macho mawili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la msingi namba 358 limetaja barabara hii ambayo inaunganisha Wilaya ya Gairo na Kilindi, swali langu la nyongeza ni kama ifuatavyo; mwaka 2010 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga barabara hii kw akiwnago cha lami. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kigua kwa sababu tumezungumza sana juu ya barabara hizi ambazo zinaunganisha Wilaya ya Kilindi na hii barabara ambayo nilikuwa nimeijibia swali kutoka Gairo kwenda Kilindi kama Mheshimiwa Kigua anavyosema ni barabara ambayo tunaitegemea siku za usoni na kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais tutaiunganisha na barabara hii muhimu ambayo kwa hatua za ujenzi zimeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu tukishaanza kufanya usanifu hata barabara hii kubwa ukitoka Handeni unapita eneo la Kibirashi ambapo ndiyo barabara hii anaitaja Mheshimiwa Mbunge, itaungana na hii barabara tukiendelea kwenda kule Chemba hadi Singida. Kwa hiyo unafahamu kabisa tuko kwenye hatua ya ujenzi wa barabara ile. Niombe uvute subira, mahitaji ya ujenzi wa barabara ni mengi, tutaenda kidogo kidogo kadri fedha zinavyoruhusu ili tuweze kuendelea kufanya ujenzi huu na ahadi itakuwa inaendelea kutekelezwa hivyo. Kwa hiyo, vuta subira barabara ile kubwa itakwenda na hii ambayo itatuunga kutoka barabara kubwa ya kutoka Dar es salaam – Morogoro kuja Dodoma kwa maana ya Gairo kwenda Kilindi itaungana na hii barabara. Tunafahamu hivyo, kwa hiyo naomba uvute subira tu, usiwahishe shughuli, siku za usoni tutakwenda kujenga barabara hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mwezi uliopita tarehe 15 Mei ilitokea ajali mbaya ikaua watu wanne papo kwa papo na wengine watano wakafa baadae na majeruhi katika Kivuko cha Daraja la Mto Una njiapanda ya kwenda *KINAPA* ambapo barabara hii ina madaraja manne na madaraja haya ni *single deck* na sio *double deck* ambayo yanasababisha ajali na hali sio nzuri.

Je, Serikali kwa udharura huu ambao barabara hii inapitisha watalii pia inayatengenezaje madaraja haya yawe na *double deck* badala ya *single deck* ili kuweza kuondoa ajali hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbatia amezungumza juu ya ajali, lakini akubaliane na mimi kwamba kunapotokea ajali yako mambo mengi, mengine ni yale makosa ambayo sisi kama binadamu tunayafanya na mengine yapo yanahusisha miundombinu, lakini *engineer* utakubaliana na mimi tafiti zinaonesha asilimia 80 ya ajali inatokana na *human behavior* (tabia za kibinadamu).

Kwa hiyo, kwanza nianze kutoa wito tu kwa watumiaji wa barabara wawe makini kwa sababu ninaamini kwamba sehemu ambayo tuna barabara hii kama unavyosema iko na *single deck* ziko alama ambazo zimeoneshwa kuchukua tahadhari, lakini wako watumiaji wachache wa barabara hawazingatii maelekezo yanayokuwa katika barabara zetu. Kwa hiyo nisisitize hilo tu watumiaji wote wa barabara wazingatie matumizi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala lako la kuitengenza barabara hii katika madaraja hayo manne

uliyoyataka kuwa *double deck* naomba nilichukue kama ushauri tuifanyie kazi tuone kwamba tunaweza kurekebisha kadri itakavyokuwa imewezekana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swali lake.

Na. 110

**Mradi wa Maji wa Mto Mbwinji Kutoa Maji kwa Vijiji na Zahanati**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Mto Mbwinji upo kwenye chanzo chenye maji ya kutosha, ambapo bomba la mradi linaloelekea Nachingwea limepita kwenye vijiji vyenye matatizo makubwa ya maji.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba la maji vinapata huduma hiyo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwahakikisha wananchi wa Ndanda kuwa zahanati na vituo vya afya vitaunganishwa na huduma hii muhimu ya upatikanaji wa maji?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda lenye sehemu (a) (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Safi wa Masasi – Nachingwea licha ya kuhudumia miji ya Masasi na Nachingwea, pia unatoa huduma ya maji katika vijiji vilivyo

kandokando ya mabomba makuu yatokayo kwenye chanzo cha Mbwinji kuelekea katika miji hiyo. Hadi sasa jumla ya vijiji 30 katika Wilaya ya Masasi, Nachingwea na Ruangwa vimeshaunganishwa na mradi huo. Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Safi Nachingwea *(MANAWASA)* itaendelea kuunganisha vijiji vyote vilivyopo kandokando ya bomba kuu ili kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kuunganisha zahanati mbalimbali na huduma za maji ambapo hadi sasa imeshaunganisha zahanati za Nangoo, Chisegu na Chikundi zilizopo Wilaya ya Masasi. Aidha, kwa zahanati za Naipanga na Mkotokuyana Wilaya ya Nachingwea, zahanati za Nandanga na Mbecha Wilaya ya Ruangwa zinapata huduma za maji katika vituo vya kuchotea maji vilivyojengwa karibu. Serikali itaendelea kuhakikisha zahanati zote pamoja na vituo vya afya vinaunganishwa na huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa pia tuyafanye yafuatayo; kwanza kabisa, chanzo cha maji cha Mbwinji kilitengenzwa maalum kabisa kwa ajili ya kusaidia Wilaya za Masasi kama ambavyo umesema, lakini hivi sasa mimi na wewe tunaongea kwa mfano, Kijiji cha Liputu ambapo bomba linalokwenda Nachingwea likitokea Kijiji cha Nangoo kilometa tano tu mpaka sasa kijiji kile hakina maji na kwamba watu wa *MANAWASA* maka leo hawajaweza kuweka maji kuwaunganishia wananchi wa pale. Je, kauli yako ni nini kuhusianan na hiki kijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwenye mpango mkubwa wa bajeti ya Wizara yako iliyoletwa hapa kwetu umeongelea kuhusu mabwawa yatakayojengwa Mihima,

Mpanyani pamoja na Chingulungulu, lakini mimi wakati nashauri Serikali nilijaribu kueleza kwamba ni bora tukafanya utafiti ili kuweza kutumia maji safi na salama yaliyopo kwenye hili bomba kubwa la Mbwinji ili kuweza kuyafikisha Lukuledi.

Sasa ningependa kujua kauli yako. Mko tayari kufanyia kazi wazo langu ili wananchi wa Kata ya Lukuledi wapate maji safi na salama badala ya kutegemea maji ya bwawa ambayo ni gharama kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri lakini kikubwa ambacho nataka kusemani, maji ni uhai na maji hayana mbadala na jukumu la kulinda uhai wa Watanzania wa mijini na vijijini tumepewa sisi Wizara ya Maji. Nataka nimhakikishie tumefanya mageuzi makubwa sana ndani ya Wizara yetu ya Maji.

Moja ni kuhakikisha kwamba eneo la kijiji ambacho kinapitiwa na bomba kuu, kilometa 12 upande wa kulia ama kushoto vinahakikishiwa vinapata huduma ya maji. Kwa kuwa vijiji hiki kiko katika kilometa tano tutamuagiza Mkurugenzi wa *MANAWASA* aangalie afanya tathmini ili tuwaangalie wananchi hawa wa Nangoo nao waweze kupata huduma hii muhimu sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la kuhakikisha katika eneo hili la Lukuledi wanapata maji ukiachana na mabwawa, sisi jukumu letu ni kuhakikisha Watanzania wanapata maji na kama kuna njia mbadala ambayo itakuwa haitumii gharama kubwa sisi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuko tayari na nipo tayari mimi mwenyewe kwenda kuona hali halisi ili mwisho wa siku tuweze kuchukua hatua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucia Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji katika Mkoa wa Njombe bado ni kubwa sana. Maeneo mengi, vijiji vingi havina maji na hata Njombe Mjini bado tatizo la maji ni kubwa, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuleta maji Njombe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara tunatambua moja ya maeneo yenye changamoto ni eneo la Njombe, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuona haja kabisa ya kutupatia fedha zaidi ya dola milioni 500 kwa miji 28. Katika miji hiyo, mmojawapo katika Mji wa Njombe.

Nataka nimhakikishie tumekwishaandika mkataba haraka kwa maana ya wahandisi washauri wapo katika maeneo mbalimbali, itakapofika mwezi wa tisa wakandarasi wote watakuwepo *site,* nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, itakapofika mwezi wa tisa wakandarasi watakuwa *site* katika utekelezaji wa mradi wa maji katika eneo la Njombe. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Masala, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwakunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya maji ambayo yametajwakatika Jimbo la Ndanda na huo mradi wa *MANAWASA* kwa sababu unahudumia Wilaya ya Nchingwea, naomba kufahamu mkakati wa Wizara wa kuhakikisha upanuzi wa miradi hii ya maji katika vijiji vya Nachingwea hasa vijiji vya Namatula pamoja na Mperuka ambako tayari

tulishaanza zoezi la kusogeza maji hayo yanayotokana na chanzo cha mto Mbwinji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Masala kwa kazi kubwa kwanza anayofanya katika Jimbo lake lakini kikubwa sisi tuna chanzo hiki cha uhakika wa maji, limebaki tu suala la usambazaji. Lakini Mheshimiwa Waziri wangu wa Maji alikwishatoa agizo kwa mamlaka hizi za maji kuhakikisha kwamba inatenga asilimia 20 ya fedha zao za mapato ili kuhakikisha kwamba wanafanya upanuzi.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara tutalisimamia hilo katika kuhakikisha vijiji vyake alivyovieleza vinapata huduma hii muhimu sana ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 360

**Kuvifufua na Kuanzisha Viwanda – Songea Mjini**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha Tumbaku cha *SONAMCU* kilichopo Songea Mjini?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha pia Kiwanda cha Usindikaji wa Samaki wanaotoka Ziwa Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ambayo ndiyo msimamizi wa vyama vya ushirika Tanzania imewezesha kukamilisha mkataba wa makubaliano ya kufufua kiwanda cha *SONTOP* kilichopo Songea Mjini kati ya Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku yaani *SONAMCU* na kampuni inayonunua tumbaku Mkoa wa Ruvuma inayoitwa *Premium Active Tanzania Limited.* Kampuni hiyo ilitoa kiasi cha dola za Kimarekani 3,050,000 kama dhamana kwa ajili ya kukifufua kiwanda hicho kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Wakulima wa zao hilo.

Vilevile vyama vyote vya msingi vimeingia m kataba na Chama Kikuu cha Ushirika - *SONAMCU* ili kudhibiti tumbaku yote inayozalishwa Songea na Namtumbo kusindikwa katika Kiwanda cha Tumbaku kilichopo Songea Mjini. Pindi kiwanda kitakapoanza uzalishaji chama hicho kitakuwa kinakatwa kiasi cha fedha kama sehemu ya marejesho kwa kampuni tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuanzisha Kiwanda cha Samaki katika mwambao wa Ziwa Nyasa ni la muhimu sana na ni sehemu ya mpango wa Serikali kupitia mpango wa uwekezaji yaani *investment guide* wa Mkoa wa Ruvuma. Wilaya ya Nyasa imetenga eneo lenye ukubwa wa hekari 345 eneo la Kilosa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda husika. Vilevile Serikali imeshaanza kuweka mazingira wezeshi ya miundombinu kwa kupeleka umeme wa uhakika wa *kilovott 33* na ujenzi wa barabara ya lami kilometa 67 kutoka Mbinga hadi Mbambabay wenye thamani ya shilingi bilioni 129, meli mbili za mizigo yaani *MV Ruvuma* na *MV Njombe* na kuimarisha mtaji nguvukazi kwa kujenga Hospitali ya Wilaya ya Nyasa na vituo vya afya kwa thamani ya shilingi takriban bilioni 3.54.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na mkoa inaendelea na jitihada ya kutafuta wawekezaji mbalimbali wakiwemo wa viwanda vya kusindika samaki. Hivi sasa Serikali kupitia taasisi zake za *SIDO* na *TAFIRI* zimekuwa zikifanya mafunzo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya awali kwa wavuvi wa eneo hilo kuhusu uvuvi, usimamizi na uzalishaji wa samaki pamoja na huduma kwa wateja *(customer care).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia *Corporate Social Responsibility* ya Mradi wa Barabara ya Mbinga – Mbamba Bay wilaya iliainisha mradi wa uwezeshaji wa kuongeza thamani mazao ya samaki wenye thamani ya takriban shilingi milioni 455 ili kuongeza tija ya mradi husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili name niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kwa majibu ya Serikali namna yalivyo. Ilikuwa tarehe 7 Februari, 2018 kwenye swali langu namba 93, niliuliza swali kuhusiana na kiwanda hiki hiki cha *SONAMCU,* majibu ya Serikali niliambiwa kwamba ikifika mwezi wa nane mwaka jana, kiwanda hiki kitakuwa kimeanza kufanya kazi, lakini mpaka leo hii ni takribani mwaka mmoja na miezi minne, kiwanda hakijaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niulize swali moja dogo la nyongeza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kwa nini Serikali inawadanganya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hususan Songea na Namtumbo?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokufanya kazi kwa kiwanda hiki, Serikali haioni kama inapoteza ajira

kwa wananchi 2500, lakini pia Serikali haioni kama inakosesha Serikali mapato? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kadri ambavyo nitachagua kama ifuatavyo, kwa sababu nimeulizwa mengi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimfahamishe Mheshimiwa Msongozi, uwekezaji katika kiwanda hicho unafanywa na sekta binafsi. Wajibu wa Serikali ni kuwezesha na kazi ambayo imefanyika. Kuhusiana na mazingira yaliyoko sasa, kwanza kabisa mwekezaji alikuwa anadai *VAT Refund* na wakati huo huo kabla ya kulipwa anastahili kuchunguzwa hapo ambapo itaonekana alichodai ndicho kiachostahili atarejeshewa na ndipo atakapowezeshwa sasa kuendelea na shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo hatuna nia ya kuwakatisha tamaa wananchi wa Songea wala Namtumbo. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, kiwanda hiki kitaendelea kuhamasishwa na kuwezeshwa ili kuweza kufikia malengo ambayo yamekusudiwa. Niwaombe sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma ambao mimi pia ni mwananchi wa Mkoa wa Ruvuma, tunayo dhamira ya dhati ya kuona kwamba, ajira zilizokuwa zinapatikana kupitia kiwanda hiki zinarejea na wananchi wananufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kama ilivyo kwa Kiwanda cha *SONAMCU* kilichopo Songea Mjini. Je, ni lini Serikali itatusaidia sisi wananchi wa Wilaya ya Rungwe kwa Kiwanda cha Chai cha Katumba ili kuongeza kiwanda kingine na kuleta ufanisi wa

utengenezaji wa chai na kuleta bei bora kwa wakulima kwa sababu kutakuwa kuna ushindani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujua Serikali itaruhusu lini kiwanda kingine kijengwe kuweza kusaidia wakulima wa chai? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi sisi tungetamani kuona viwanda vingi vinajengwa na vinaweza kuchakata mazao ya wananchi na kwa tija. Kwa hiyo, kadri viwanda vinavyojengwa, sisi ndiyo tunavyofurahi, kwa hiyo, hatujazuia kiwanda kingine kujengwa Katumba na kilichopo tungependa kiweze kufanya kaz vizuri zaidi. Kwa hiyo, kama kuna kikwazo chochote ambacho kinawakabili hawa Wana Katumba, ni vema tufahamishwe ili tuweze kushirikiana nao katika kuondoa vikwazo hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Ngonyani, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, naomba nirudi tena pale kwenye Kiwanda cha *SONAMCU*, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba changamoto iliyopo kwa kutotekeleza ule mkataba, ni kwa Serikali kutowarudishia wale wanunuzi haki yao ambayo ni *VAT return* na kama mnakumbuka Mheshimiwa Rais aliliongelea hilo juzi kwamba inaonekana Wizara ya Viwanda haifanyi jitihada yoyote ya kuwasaidia wawekezaji kuondokana na changamoto zao.

Je, sasa Wizara ya Viwanda na Biashara imejifunza na iweze kutatua changamoto hiyo ya *VAT return* kwa kampuni inayonunua tumbaku Songea ili iweze kujenga kile kiwanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama nilivyosema hapo awali, hizi *VAT return* haidaiwi na kiwanda cha *SONAMCU* peke yake, kuna wadau wengi ambao walidai, wengine wamerejeshewa, wengine bado wapo katika mchakato wa uhakiki.

Nipende tu kusema kwamba, kimsingi Serikali ina dhamira njema ya kurejesha *VAT returns* lakini, baadhi ya waliodai, wengine hawakutoa taarifa ambazo ni sahihi, na hiyo imepelekea kufanya zoezi hili kuwa kubwa kwa kuhakiki wale wote ambao walikuwa wanadai *VAT returns* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Wizara inao wajibu wa kuendelea kujifunza lakini kuendelea kutatua changamoto ambazo wote tunaona kwamba ni za msingi. Tunayo dhamira njema na niseme tu kwamba katika maeneo ambayo tutafuatilia ni pamoja na Kiwanda hiki cha *SONAMCU* Songea.

**NAIBI SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 361

**Mpango wa Kuwarejesha wakimbizi makwao**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Baadhi ya magereza nchini yamejaa wafungwa na mahabusu ambao ni wakimbizi.

Je, ni lini Serikali itawarejesha wakimbizi hao makwao ili kupunguza msongamano ndani ya magereza yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba miongoni mwa wafungwa na mahabusu walioko katika magereza hapa nchini ni raia wa kigeni wakiwemo wakimbizi kutoka nchi za Burudi, DRC na nchi nyingine duniani. Magereza yenye idadi kubwa ya raia wa kigeni yapo Mkoani Kigoma ambapo yana jumla ya wakimbizi 91 kati yao wafungwa 38 na mahabusu 53. Gereza la Kibondo lina wafungwa 22 na mahabusu 31, Gereza la Kasulu lina wafungwa wawili na mahabusu 19, Gereza la Bangwe lina mfungwa mmoja na mahabusu watatu, Gereza la Ilagala lina mfungwa mmoja na Gereza la Kwitengo lina jumla ya wafungwa 12. Wakimbizi ambao wamefungwa gerezani wanarejeshwa katika nchi zao za asili baada ya kumaliza kutumikia vifungo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea kuwarejesha wakimbizi nchini kwao kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi *(UNHCR),* Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wahamiaji *(IOM)* pamoja na nchi ya Burundi. Kuanzia mwezi wa Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 jumla ya wakimbizi 31,643 kutoka Burundi walirejeshwa nchini kwao kwa hiyari.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi hiyo imefanya wakimbizi waliorejeshwa nchini mwao tangu zoezi hilo lilivyoanza mwaka 2017 hadi 2019 kufikia 66,148. Aidha, zoezi la kuwarejesha wakimbizi hao nchini kwao kwa hiari ni endelevu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rukia Ahmed, swali la nyongeza.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakimbizi kutoka Somalia pamoja na wakimbizi kutoka Ethiopia, hawawezi kuingia nchini mpaka wapitie nchi ya Kenya. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja kwa kushirikiana na nchi ya Kenya kuwazuia wakimbizi hawa wasiingie katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa ukiacha wakimbizi walioko katika magereza, kuna wakimbizi ambao wako katika kambi za wakimbizi. Kwa mfano, Kadutu - Kigoma, Ulyankulu - Tabora pamoja na kambi nyingine. Wakimbizi hawa wana tabia ya kuzaana sana na kwa kweli idadi yake inaongezeka ukizingatia miaka 10 iliyopita sasa hivi wako mara mbili zaidi.

Je, Serikali, kwa kuwa nchi zao tayari zina amani, wana mkakati gani wa kuwarejesha wakimbizi hawa ili wasiendelee kuzaana hapa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na rai yake ya kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba rai yake ambayo ameitoa tumeshaanza kuifanyia kazi. Hivi karibuni tulikuwa tuna kikao kilichoshirikisha ngazi ya Mawaziri wa Tanzania, Kenya na Ethiopia, ili kujadiliana namna ya pamoja ya kudhibiti wimbi la wahamiaji hawa hususan wanaotokea Ethiopia ambao wanaingia kwa wingi kupitia Kenya na jambo hilo limeleta mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala la wakimbizi kurudi makwao, kama ambavyo nimejibu swali langu la msingi kwamba kwa takwimu za mpaka Aprili, 2019 tuna zaidi ya wakimbizi 99,000 ambao wameamua kurudi kwa hiari. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba nalo hili ni jambo ambalo tumeshaanza kulifanyia kazi na tunaendelea nalo. Kwa sababu ni kweli kama alivyozungumza Mbunge kwamba hali ya amani katika nchi hizi imetulia, hakuna sababu ya

wakimbizi hawa kuendelea kubaki katika nchi yetu kwa kipindi hiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini.

Na. 362

**Hitaji la Kituo cha Polisi Makao Makuu ya Wilaya - Tanganyika**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. MOSHI S. KAKOSO)** aliuliza:-

Wilaya ya Tanganyika haina Jengo la Polisi Makao Makuu ya Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi eneo la Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Anna Lupembe! Mheshimiwa Anna Lupembe inabidi uzungumze tena kwa sababu inabidi nikuruhusu kuongea ndiyo uongee, kwa sababu umeongea kabla, kwa hiyo, uliza sasa swali kwa niaba ya Mheshimiwa Moshi Kakoso.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. MOSHI S. KAKOSO)** aliuliza:-

Wilaya ya Tanganyika haina Jengo la Polisi Makao Makuu ya Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi eneo la Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:**Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa Wilaya mpya zilizoanzishwa na Serikali katika miaka ya hivi karibuni ambazo hazina vituo vya polisi na hata nyumba za kuishi askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua hitaji la Kituo cha Polisi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Tanganyika na mpango wa kujenga Vituo vya Polisi katika Makao Makuu ya Wilaya yataanza mara baada ya kufanyika kwa tathmini ya eneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Tanganyika ni jiografia yake ni ngumu sana na Makao Makuu ya Wilaya yako Majalila, lakini *OCD* anakaa Mishamo na ukizingatia jiografia ile ni pana sana, watu wa Karema wanashindwa kwenda Mishamo.

Je, Serikali itaweka mikakati gani kuhakikisha basi kile kituo cha polisi hata kama bado fedha hazijapatikanika, lakini kituo kiwekwe *center* ili watu wote katika Wilaya ile waweze kujua kituo chao cha polisi kiko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na jiografia mbaya ya Wilaya ya Tanganyika, je, ni lini Serikali itatuletea magari ya polisi kwa ajili ya *patrol* kwa sababu kuna misitu mingi, mikubwa sana katika wilaya ile, sasa majambazi wako wengi na uhalifu unafanyika mara kwa mara. Serikali itatuletea lini magari kwa ajili ya *patrol* ya Wilaya yetu ya Tanganyika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hoja ya Mheshimiwa Lupembe ni ya msingi, na kwa kuzingatia msingi wa hoja yake, sasa tutalifuatilia kwa karibu tuone lile eneo ambalo Halmashauri imekusudia kulitenga kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi, liwe Majalila kama ambavyo amependekeza ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya. Sambamba na ule ujenzi wa nyumba nne ambazo mchakato wake unaendelea wa ujenzi katika eneo hilo la Wilaya ya Tanganyika, liende sambamba pamoja na rai ambayo Mheshimiwa Mbunge ametoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusianana na magari nayo, kwa sasa hatuna magari mapya ambayo yameingia, lakini kwa kutambua umuhimu wa jiografia ya Tanganyika kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, basi suala lake tumelichukua na pale ambapo magari yatapatikana basi tutazingatia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

Na. 363

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Eneo la Magereza Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Eneo la Rubwera Kata ya Kyerwa ndiyo Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengi yalikuwa ya wananchi, kuna eneo lilichukuliwa na Jeshi la Magereza na wananchi walizuiliwa kufanya shughuli yoyote kwenye eneo hilo.

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hawa kama walivyoahidiwa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wakati wa uanzishwaji wa Wilaya mpya ya Kyerwa, eneo la wananchi wa Kijiji cha Rubwera Kitongoji cha Rwekorongo lilitolewa kwa ajili ya uanzishaji wa Gereza la Wilaya. Aidha, kwa mujibu wa tathmini ya Halmashauri ya Wilaya, jumla ya shilingi 661,928,640/= zinahitajika kuwafidia wananchi waliojitolea maeneo yao mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuwalipa fidia wananchi wote nchini waliotoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha ujenzi na au uanzishaji wa magereza ikiwemo wananchi wa Rubwera. Aidha, Serikali itaendelea kulipa fidia hizo kwa wananchi kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha kutoka kwenye bajeti ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nisikitike sana kwa majibu ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uthaminishaji wa maeneo yale umefanyika zaidi ya miakakaribia miaka minne, na kwa mujibu wa sheria inabidi warudi tena kufanya uthaminishaji upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wameshindwa huu wa kwanza kulipa, watawezaje kufanya uthaminishaji wa awamu ya pili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, mko tayari kuwatangazia wananchi wa Rwenkorongo pale Kyerwa kuwa mmeshindwa kuwalipa ili waweze kuendeleza maeneo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu inaonesha moja kwa moja mmeshindwa kuwalipa wananchi, mko tayari kuongea na Halmashauri ili iwatafutie maeneo mengine ambayo hayatahitaji fidia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijashindwa kulipa fidia wananchi na Serikali ina nia ya kulipa fidia wananchi. Kama ambavyo nimezungumza katika majibu yangu ya msingi, ni kwamba fidia hizi, maeneo haya ni mengi ambayo yanahitaji kulipwa fidia na suala hili haliwezi likafanyika kwa wakati mmoja.

Kwa hiyo, ninalirudia jibu langu la msingi ambalo nimejibu kwamba fidia za eneo hili ambalo lilichukuliwa kwa ajili ya magereza na maeneo mengine, najua kuna Waheshimiwa Wabunge ambao maeneo yao mengine vilevile yanahitaji kulipwa fidia, zitalipwa kwa awamu kadri hali ya kifedha na kibajeti itakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali la mwisho la Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 364

### Hitaji la *MRI* Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka kipimo cha *MRI* katika Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziriwa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwongozo uliokuwepo huduma za *CT-Scan* na *MRI* hazikuwepo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Hata hivyo, kufuatia mabadiliko ya kiuchumi na uhitaji wa huduma hizi kwa wananchi, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilifanya mabadiliko ya mwongozo kwa kutengeneza mwongozo mpya wa vifaa vya Radiolojia nchini wa mwaka 2018 *(Standard Medical Radiology and Imaging Equipment Guidelines)* ambapo pamoja na mambo mengineyo huduma za *CT-Scan* na *MRI* zitapatikana katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa na huduma za *MRI* zitapatikana katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko hayo Serikali inakusudia kufunga *CT-Scans* katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwa ni Mwananyamala, Temeke na Amana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ninaridhika nayo na ninaipongeza Serikali kwa

kupandisha hadhi Hospitali hizo za Ilala, Amana, Mwananyamala na Temeke, kwa kweli hosptali hizo zimekuwa msahada mkubwa na tumepunguza sana *route* za kwenda Muhimbili na Mloganzila.

Swali langu sasa kwa kuwa katika hospitali hizo za Mkoa hazina hizo mashine za *MRI* jambo ambalo linasababisha msongamano mkubwa wa kupata huduma hiyo katika Hospitali ya Muhimbili. Je, Serikali inautaratibu gani wa kupunguza foleni ya kupata kipimo hicho katika Hospitali ya Muhimbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam una Wilaya mpya za Kigamboni na Ubungo ambazo Wilaya ya Kigamboni wanatumia Hospitali ya Vijibweni kama Hospitali ya Wilaya na Wilaya ya Ubungo wanatumia Hospitali ya Sinza Palestina kama Hospitali ya Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma mbalimbali ikiwemo hizo za mashine za *x-ray* na mashine nyingine katika hospitali hizo ambazo zinawasaidia wananchi wa Kigamboni na wananchi wa Wilaya ya Ubungo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhemiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam, amekuwa ni chachu ya kufuatilia mambo mengi ya Mkoa wa Dar es Salaam ni mfano wa kuigwa Wabunge wa Viti Maalum kwa sababu amekuwa ametupa ushirikiano mkubwa sana sisi Wabunge wa Majimbo ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tuliona mahitaji ya huduma ya *CT-Scan* na *MRI* yanazidi kukua kutokana na hali ya mabadiliko ya wagonjwa na nitoe tu historia kwa sababu miaka ya nyuma

tulikuwa na changamoto ya magonjwa ya kuambiza, sasa hivi tuna matatizo ya magonjwa yasiyoambukiza ambapo huduma hizi za *CT-Scan* na *MRI* zinahitajika sana. Na kwa mwanzo tulikuwa tumeanza katika Hosptali za Rufaa za Taifa na Kanda, lakini kutokana umuhimu wa huduma hizi za *CT-Scan* na *MRI* ndiyo maana sisi kama Serikali tumesema sasa tunataka tuziweke katika ngazi ya Rufaa ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kupunguza tatizo la foleni la huduma ya *CT-Scan* pale Muhimbili ndiyo maana sasa sisi tumekusudia kuhakikisha kwamba huduma hizi zinapatikana katika Hospitali za Rufaa za Amana, Mwananyamala pamoja na Temeke na hilo ndilo kusudio letu na mchakato tumeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swala lake la pili ameuliza jinsi gani tunaweza tukapanua wigo wa huduma hizi katika hospitali nyingine hususani katika zile za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii naomba niliseme kwamba tunajenga Hospitali hizi za Wilaya moja pale Kigamboni, vilevile kule katika Wilaya ya Ilala. Lakini na mimi niombe niseme kwa sababu moja ya hoja ambayo umeigusia hapa ni katika Jimbo langu ambalo na mimi ni mwakilishi wa wananchi na niseme hivi tunavyoongea leo tunazindua huduma za *x-ray* katika Hospitali ya Vijibweni na nitoe rai kwa wananchi wa Kigamboni kwenda katika Hospitali ya Vijibweni huduma ya *x-ray* sasa inaanza kupatikana kuanzia leo.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Sasa nitaleta matangazo kwenu, tuliyonayo hapa mezani.

Tangazo la kwanza linahusu wageni kwanza, tunaanza na wageni walioko Jukwaa la Mheshimiwa Spika, nao ni wageni wanne wa kwangu ambao ni Waheshimiwa Madiwani wawili kutoka Jiji la Mbeya na hawa wameambatana na wapiga kura wao, Mheshimiwa Daudi Ngogo, Diwani wa Kata wa Nsalaga na Mheshimiwa Newton Mwatujobe. Hawa wameambatana na wapiga kura wao

Ndugu Shikunzi Zinzendofu na Ndugu Manase Sanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni mbalimbali tukianza na kundi la wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga - Waziri wa Kilimo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimbo la Vwawa Mkoa wa Songwe Ndugu Hemed Kibona. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni kikundi cha *MAESO* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa kikundi hicho Ndugu Dominatha John, siwaoni wakisimama kwa hiyo naamini hawakupata nafasi pengine ya kuingia Bungeni, ahaa wako wawili sio wanne tena karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Anatropia Theonest ambao ni rafiki zake kutoka Segerea, Jijini Dar es Salaam huyu ni Ndugu Faustine Mwangamila na Ndugu Abiasi Mkude, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambaye ni mpiga kura wake kutoka Mbulu, Mkoa wa Manyara na huyu ni Ndugu Malliadi Lohay, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Aisharose Matembe ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dodoma na huyu ni Ndugu Naomi David, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kutoka Busanda Mkoa wa Geita ambaye ni Mwalimu Mchungaji Sikujua Mbatilo karubi sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wengine 39 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Kwaya ya Shalom kutoka kanisa la *African Inland Church* la Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbaimbali waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo; kundi la

kwanza ni wanafunzi 100 na walimu 10 kutokao shule ya sekondari Itega ya hapa Jijini Dodoma, wakiongozwa na Mwalimu Grace Mabula, haya labda wako *basement*. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanafunzi 150 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi Kizota iliyopo Jijini Dodoma karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 27 na walimu watatu kutoka *Mwenge Catholic University* cha Mjini Moshi wakiongozwa na Ndugu Elibariki Sinda, karibuni sana.*(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili kutoka Jijini Dodoma ambao ni Ndugu Mary Leonard na Ndugu Methew Chalia, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulionao siku ya leo lakini ia wapo wageni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Kwaya ya Nuru kutoka Kanisa la Anglikana Parish ya Mlimwa Mjini, karibuni sana wanakwaya, lakini pia ipo kwaya ya Shalom kutoka Kanisa la *AICT* Kizota, sasa hawa nadhani ni wageni wa Wabunge wawili Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo kutoka Idara ya Utawala la Rasilimaliwatu, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Maafisa kutoka Idara ya Uhamiaji wapo hapa Bungeni kwa ajili ya kutoa hati mpya za kusafiria yaani *passport* za kielektroniki kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliojisajili kwa ajili ya kupatiwa hati hizo, zoezi la utoaji wa hati hizo linafanyika katika Ukumbi Namba 9 Jengo la Utawala karibu na chumba cha maslahi, hivyo Wabunge wote waliokuwa wamejiandikisha wanaombwa kufika ili wachukue hati zao ambazo zinatolewa kuanzia leo.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake, anawatangazia Wabunge wote sio Wabunge Wanawake peke yao, lakini

Wabunge wote mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kutakuwa na kumsikiliza Spika kutoka Rwanda atakuwa akizungumza na Waheshimiwa Wabunge wote Ukumbi wa Msekwa, Wabunge wote mnakaribishwa kwenda huko kumsikiliza huyu mwanamama mahiri kabisa kutoka Rwanda ambaye jana ulisomwa wasifu wake hapa na Mheshimiwa Spika na pamoja na hayo na kwa umuhimu mzito kabisa Bunge la Rwanda lina wanawake asilimia 61.3. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wabunge wanaume mnakaribishwa sana ili mkajifunze kwamba huko kwa wenzetu wanaume wanafanyaje mpaka wanawake wanakuwa wengi Bungeni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenda kumsikiliza Mheshimiwa Donatille.*(Makofi)*

Lipo pia tangazo lingine la ibada kutoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa Ibada *Chapel* ya Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo siku ya Jumanne saa saba mchana badala ya saa tano kama ilivyokuwa imetangazwa hapo awali kutakuwa na ibada ambapo Ibda hiyo Mtumishi Eliamini Mbaga kutoka Dar es Salaam atahudumu.

Kkwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tukitoka kumsikiliza Mheshimiwa Spika kutoka Bunge la Rwanda basi mnakaribishwa kwenye Ibada na Mheshimiwa Anna Lupembe.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa ujumbe hapa na Mheshimiwa Keissy kwamba ana jambo la dharura, nitampa fursa yeye kumsikiliza halafu tutafanya uamuzi. Mheshimiwa Ally Keissy.*(Makofi)*

## HOJA YA DHARURA

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante natoa mwongozo kwa kanuni ya 47(2) na 50(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sana tumekatwa pesa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya mfano na

watu wakaenda kule *Mlimani City* wakacheza, lakini mpaka leo mimi nikisema ni sababu ni mitandao leo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanasema nimekaa kimya na baadhi ya Wabunge wanasema nimekula rushwa au nimepewa ya kujengewa choo. Ni kitu cha ajabu ni muda mrefu zaidi karibu ifike mwaka hakuna taarifa yoyote iliyotolewa hapa Bungeni, wala kujua lolote tumepata kiasi gani cha pesa wala pesa ziko wapi hizo pesa tulizochanga, hatuna taarifa yoyote wamekaa kimya na wamejitahidi kwenye mitandao lakini hakuna jibu lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na kipindi cha Bunge kinakaa saa 12 jioni karibu tumalize Bunge, hatuna taarifa yoyote na hatuna mpango wowote wa ujenzi wa hivyo vyoo. Tunaomba kama wameshindwa waturudishie pesa zetu kila Mbunge kwenye Jimbo tukafanye mambo mengine ya kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hoja Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, tuchangie. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, amesimama Mheshimiwa Keissy kwa mujibu wa Kanuni ya 47; Kanuni inayozungumza kuhusu kuhairisha shughuli za Bunge ili kuweza kujadili jambo la dharura.

Kwa maelezo yake Mheshimiwa Keissy ambayo sikusudii kuyarudia ameeleza kuhusu michango iliyotolewa si na Wabunge pekee, lakini pia na wadau mbalimbali ambao walipata fursa ya kutuchangia ili tuweze kujenga vyoo vya mfano katika Majimbo yote ya Tanzania Bara, lakini pia na Majimbo ya Tanzania Visiwani kwa maana ya Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, kwa masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 47 lakini pia Kanuni ya 48, jambo hili si kwamba ni la dharura kwa sababu halijajitokeza kwa muktadha wa Kanuni ya 47 na 48 kwa sababu masharti yaliyowekwa katika Kanuni hizi yanataka jambo hilo ambalo Bunge linaweza kulijadili kwa kutumia Kanuni hii liwe ni lile ambalo haliwezi kufanyiwa kazi katika utaratibu wa kawaida.

Lakini hata hivyo nilikuwa nimemuona Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake akiwa amesimama, sitampa fursa ya kuzungumza, lakini jambo hili Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka Mheshimiwa Spika ndiye aliyekuwa akilisimamia, kwa hiyo liko mikono salama, fedha ziko mikono salama tusitie shaka, wakati utakapofika wa kutoa mrejesho wa namna ya hili zoezi litakavyofanywa kwenye Majimbo basi Bunge litawatangazia kama ambavyo liliwatangazia kuhusu mpango wa huo kukusanya hizo fedha kwa ajili ya ujenzi wa hivyo vyoo. *(Makofi)*

Nichukue fursa hii kuwakumbusha wadau wetu wote waliokuwa wameahidi ambao hawajakamilisha ahadi zao wakamilishe ili Bunge liweze kuendelea na utaratibu wake lililokuwa limejiwekea wakujenga vyoo vya mfano katika Majimbo yote Tanzania. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahiirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4:35 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 12 Juni, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*